**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**

# MWONGOZO WA MAVAZI YA WANAFUNZI KATIKA VYUO VYA AFYA KADA ZA KATI TANZANIA BARA

**Septemba, 2020**

ISBN: 978-9976-5561-1-7





# YALIYOMO


DIBAJI ........ ii

SHUKRANI ........ iii

1. UTANGULIZI ........ 1

2. LENGO LA MWONGOZO WA MAVAZI ........ 1

3. NGUO ZINAZORUHUSIWA ........ 2

3.1 Kwa wasichana/wanawake ........ 2

3.2 Kwa wavulana/wanaume ........ 2

3.3 Nguo za kujikinga na baridi zinazoruhusiwa kwa jinsia zote ........ 3

4. NYWELE ZINAZORUHUSIWA ........ 3

4.1 Kwa wasischana/wanawake ........ 3

4.2 Kwa wavulana/ wanaume ........ 3

5. UREMBO UNAORUHUSIWA ........ 4

6. VIATU VINAVYORUHUSIWA ........ 4

7. MAVAZI YASIYORUHUSIWA ........ 4

7.1 Mavazi yasiyoruhusiwa kwa wasichana/ wanawake ........ 4

7.2 Mavazi yasiyoruhusiwa kwa wavulana/wanaume ........ 5

8. NYWELE ZISIZORUHUSIWA ........ 5

9. UREMBO USIORUHUSIWA ........ 5

10. VIATU VISIVYORUHUSIWA ........ 5

11. ATHARI ZINAZOTOKANA NA KUVAA MAVAZI YASIYO NA HESHIMA ........ 6

12. MAKOSA YA KUKIUKA TARATIBU ZA MAVAZI NA HATUA ZA KINIDHAMU ........ 7

## DIBAJI

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ina jukumu la kuandaa Miongozo na kusimamia utekelezaji wake katika sekta ya Afya. Katika kutekeleza jukumu hili Wizara imeandaa Mwongozo wa mavazi ya wanafunzi wa vyuo vya afya kada za kati nchini.

Mwongozo huu utatumika kuhakikisha mavazi yanayovaliwa na wanafunzi vyuoni ni yenye staha na nidhamu. Hii imekuwa ni moja ya kipaumbele cha kitaifa kuhakikisha kila Taasisi ya mafunzo inasimamia maadili ipasavyo.

Ni matarajio ya wizara na wadau wote wa afya kuwa ikiwa Mwongozo huu utazingatiwa na pande zote basi vyuo vitakuwa si sehemu tu ya kufundisha taaluma bali pia ni eneo ambalo tamaduni na maadili ya utumishi wa umma vitarithishwa kwa wahitimu.

Prof. Mabula Mchembe

**KATIBU MKUU**

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,**

**JINSIA, WAZEE NA WATOTO**

## SHUKRANI

Uandaaji wa mwongozo wa mavazi katika vyuo vya afya vya kada za kati Tanzania bara ni matokeo ya juhudi thabiti za wadau mbalimbali wa mafunzo ya Afya nchini katika kuimarisha nidhamu katika mazingira ya kujifunzia.

Ingawa siyo rahisi kuwataja wote walioshiriki katika kuandaa mwongozo huu, shukrani za dhati ziende kwa; Dkt. Loishooki S. Laizer, Dkt. Fadhili M. Lyimo, Bw. Martin Mapunda, Dkt. Mabula Masunga Ndimila, Bw. Nassania Shango na Bi Esther Msechu, Dkt. Melkzedeck Mansi, Bw. Ndemetria Vermand, Dkt. Geofrey Mdede, Dkt. Hyasinta Jaka, Bi. Anande Mungure, Dkt. Betson Bonny, Dkt. Joseph Mwabusila, Dkt. Humphrey Shayo, Lilian Wilfred, Sarah Fares,Victor Mwambije, Dkt. Wilson Kitinya na Dkt. Mary Rose Giattas ambao kwa uzoefu wao katika kusimamia mafunzo waliweza kukamilisha mwongozo huu.

Mwisho, Wizara inatambua mchango wa wadau wote kwa kukamilisha mwongozo huu, kwa wote hao tunasema ahsante sana.

Prof. Abel Makubi

**MGANGA MKUU WA SERIKALI**

## 1. UTANGULIZI

Wizara ina jukumu la kuhakikisha upatikanaji wa rasilimali watu katika sekta ya Afya yenye maadili na weredi wa kutoa huduma za afya zinazo kubalika kwa jamii. Katika kusimamia hilo imeonekana kuna umuhimu wa kuandaa mwongozo wa kusimamia nidhamu katika mavazi.

Kufuatia ziara za usimamizi shirikishi katika vyuo vya mafunzo, imebainika baadhi ya wanafunzi kuvaa mavazi yasiyokubalika katika jamii. Hali hii inachangiwa zaidi na kutokuwepo kwa Mwongozo wa Mavazi katika Vyuo vya Afya kada za kati. Hivyo, maandalizi ya mwongozo huu yamezingatia maudhui kutoka katika kitabu cha Mwongozo wa Mavazi kwa Watumishi wa Umma na pia uchukuaji wa hatua za kinidhamu kwa wanafunzi wanaokiuka mwongozo huu utazingatia kanuni na sheria zilizopo katika kitabu cha Mwongozo wa Nidhamu kwa Wanafunzi waliopo katika Vyuo vya Afya vya kada za kati nchini.

## 2. LENGO LA MWONGOZO WA MAVAZI

Mwongozo huu unalenga katika kuhakikisha kuwa wanafunzi wote waliopo katika vyuo vya Afya vya kada za kati wanavaa mavazi yenye staha kama inavyoelekezwa katika mwongozo huu. Mwongozo huu utasaidia kuwaandaa wahitimu kuzingatia maadili ya kitaaluma na utumishi wa Umma.

## 3. NGUO ZINAZORUHUSIWA

Nguo zinazoruhusiwa kwa wanafunzi ni kama ifuatavyo:

### 3.1 Kwa wasichana/wanawake

a) Wavae sketi au gauni isiyo ya kubana, kitambaa kisichokuwa angavu (transparent) na iwe ndefu ya kuvuka magoti akiwa amekaa

b) Kuvaa sare pamoja na kitambulisho wakati wote wa masomo; darasani, wodini na maeneo ya mazoezi kwa vitendo ndani na nje ya chuo

c) Sare:

- Sare za wauguzi: Wavae gauni ya mikono mifupi yenye rangi na mtindo uliochaguliwa na Baraza la Uuguzi na Ukunga.
- Sare kwa kada za vyuo vya Sayansi Shirikishi: Gauni nyeupe ya mikono mifupi isiyokuwa na urembo (ribbon)

d) Nguo zilizoruhusiwa katika maeneo ya mazoezi kwa vitendo (mfano; koti jeupe)

e) Nguo safi na zilizopigwa pasi

f) Nguo za michezo na fulana zilizochaguliwa na taasisi/ serikali ya wanafunzi

g) Uvaaji wa soksi ndefu za aina moja zenye rangi nyeupe

h) Hijabu iwe ya rangi nyeupe na iwe fupi inayoingizwa kwenye sare

### 3.2 Kwa wavulana/wanaume

a) Kuvaa suruali ndefu zisizo za kubana na kuchomekea, kufunga mkanda kiunoni na kuvaa kitambulisho wakati wote wa masomo; darasani, wodini na maeneo ya mazoezi kwa vitendo ndani na nje ya chuo

b) Sare:

- Sare za wauguzi: Wavae shati na suruali yenye rangi na mtindo uliochaguliwa na Baraza la Uuguzi na Ukunga.
- Sare kwa kada za vyuo vya Sayansi Shirikishi: Suruali ya khaki na shati jeupe lenye mikono mifupi.

c) Nguo zilizoruhusiwa katika maeneo ya mazoezi kwa vitendo (mfano; koti jeupe)

d) Nguo safi zilizopigwa pasi

e) Nguo zinazoendana na rangi iliyochaguliwa na taasisi/Baraza la taaluma

f) Nguo zenye mtindo wa kushona uliopitishwa na taasisi/Baraza la taaluma

g) Nguo za michezo na fulana zilizochaguliwa na taasisi/ serikali ya wanafunzi

h) Uvaaji wa soksi za aina moja zenye rangi nyeupe

i) Fulana(Vest/T-Shirt) inayovaliwa ndani ya shati iwe yenye rangi nyeupe

### 3.3 Nguo za kujikinga na baridi zinazoruhusiwa kwa jinsia zote

**a)** Sweta lenye rangi nyeupe

**b)** Kwa vyuo vilivyoko kwenye mikoa yenye baridi kali wanafunzi wanaruhusiwa kuvaa mavazi ya nyongeza juu ya sare ya chuo mfano skafu nyeupe na koti lenye rangi nyeupe

## 4. NYWELE ZINAZORUHUSIWA

Nywele zinazoruhusiwa kwa wanafunzi ni kama ifuatavyo:

### 4.1 Kwa wasichana/wanawake

a) Nywele fupi za asili za kuchana na kitana

b) Nywele ndefu za asili zifungwe kwa vibanio kuelekea kisogoni ili sura ionekane na zisiachwe kuning'inia

c) Nywele za asili za kusuka kwa msitari(kuanzia mbele kwenda nyuma) bila kuweka rasta

### 4.2 Kwa wavulana/ wanaume

a) Nywele fupi za asili zinazolingana za kuchana na kitana

## 5. UREMBO UNAORUHUSIWA

Urembo unaoruhusiwa kwa wanafunzi ni kama ifuatavyo:

a) Pete za ndoa

b) Kucha fupi

c) Saa

d) Miwani kwa wenye matatizo ya macho

e) Kofia kwa wenye matatizo ya ngozi (Albino)

## 6. VIATU VINAVYORUHUSIWA

Viatu vinavyoruhusiwa kwa wanafunzi ni kama ifuatavyo:

a) Viatu vyeusi vyenye kisigino kifupi kisichotoa sauti wakati wa kutembea sakafuni.

b) Viatu vya michezo wakati wa michezo

## 7. MAVAZI YASIYORUHUSIWA

### 7.1 Mavazi yasiyoruhusiwa kwa wasichana/ wanawake

a) Nguo zinazobana

b) Nguo (gauni/sketi) fupi zinazoacha magoti wazi au mpasuo unaoonesha maungo ya ndani ya mwili

c) Nguo zinazoacha sehemu ya mwili wazi kama kitovu, kifua, mabega na mgongo

d) Nguo zinazoonyesha maungo/ nguo za ndani (transparent)

e) Nguo zilizokunjamana (Hazikunyooshwa)

f) Nguo chafu (Hazikufuliwa)

g) Nguo zilizochanika/kufumuka zipu au vifungo

h) Nguo zisizoendana na rangi zilizopendekezwa kwenye fomu ya kujiunga chuoni

i) Nguo zisizoendana na mtindo uliopendekezwa kwenye fomu ya kujiunga chuoni

j) Nguo ambazo zina picha, michoro, na maandishi ambayo hayaendani na shughuli za chuo

k) Kaptula aina yoyote ile

l) Suruali zilizofumuliwa (zilizotobolewa) au kuchanwachanwa

m) Kuvaa khanga/kitenge nje ya bweni

n) Kuvaa nguo za kulalia (night dress) nje ya bweni

o) Nguo yenye maandishi ya chama chochote cha siasa au ushabiki wa kitu fulani

p) Nguo yoyote inayopingana na maadili ya utumishi wa umma

### 7.2 Mavazi yasiyoruhusiwa kwa wavulana/wanaume

a) Suruali aina ya kadeti au jeans kutumika kama sare (hata kama ni ya rangi ya khaki)

b) Suruali za kubana

c) Shati la kubana

d) Kuvaa suruali mlegezo

e) Nguo zinazoacha sehemu ya mwili wazi kama kitovu na kifua

f) Kufunga vifungo vichache vya shati ili kifua kionekane

g) Nguo zilizochanika/kufumuka zipu au vifungo

h) Nguo zisizoendana na rangi zilizopendekezwa kwenye fomu ya kujiunga chuoni

i) Nguo zisizoendana na mtindo uliopendekezwa kwenye fomu ya kujiunga chuoni

j) Suruali yoyote fupi au iliyoachwa bila kupindwa chini

k) Kaptula ya aina yoyote

l) Nguo yenye maandishi ya chama chochote cha siasa au ushabiki wa kitu fulani

m) Nguo yoyote inayopingana na maadili ya utumishi wa umma

## 8. NYWELE ZISIZORUHUSIWA

a) Nywele chafu ambazo hazikutengenezwa vizuri

b) Nywele bandia au zilizopakwa rangi

c) Kufuga nywele ndefu kwa wavulana/wanaume

d) Kusuka rasta au mtindo wowote wa nywele za kuning'inia

e) Unyoaji nywele kwa mitindo isiyofaa

f) Kufuga ndevu

## 9. UREMBO USIORUHUSIWA

a) Hereni, Bangili na Mikufu

b) Kunyoa nyusi

c) Kupaka rangi za midomo na macho

d) Kufuga kucha ndefu na upakaji rangi kwenye kucha

e) Uvaaji wa kucha na kope za bandia

f) Meno ya urembo hayaruhusiwi

## 10. VIATU VISIVYORUHUSIWA

a) Kandambili pamoja na makobazi katika maeneo ya kujifunzia

b) Viatu vya michezo pamoja na raba (isipokuwa wakati wa shughuli maalum za michezo)

c) Viatu vya rangi isiyopendekezwa kwenye fomu ya kujiunga chuoni

d) Kuvaa viatu bila socks

e) Viatu vyenye kisigino kirefu

f) Viatu vyenye kutoa sauti kwenye sakafu

## 11. ATHARI ZINAZOTOKANA NA KUVAA MAVAZI YASIYO NA HESHIMA

- Kujivunjia heshima kwa jamii inayomzunguka
- Wagonjwa/ wateja kupoteza imani na kukataa kuhudumiwa na wanafunzi.
- Kushusha hadhi ya taaluma za afya kwa sababu wanafunzi wanaandaliwa kuwa Watumishi wa Umma na kioo kwa jamii.
- Kuzidhalilisha taasisi wanazosoma wanapokuwa kwenye jamii.
- Kuhatarisha usalama wa afya zao, wanapokuwa kwenye mafunzo


## 12. MAKOSA YA KUKIUKA TARATIBU ZA MAVAZI NA HATUA ZA KINIDHAMU

Jedwali hili linaonesha aina za makosa na hatua za kinidhamu zitakazochukuliwa:-

| Na | Aina ya kosa | Kosa la kwanza | Kosa la pili | Kosa la tatu |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Kuvaa nguo fupi na zinazobana | Kuondolewa darasani au eneo la mafunzo na karipio kali mbele ya kamati ya nidhamu | Onyo kwa maandishi kupitia kamati ya nidhamu | Kusimamishwa masomo kupitia kamati ya nidhamu |
| 2 | Kutokuvaa sare na kitambulisho awapo darasani, wodini au maeneo ya mazoezi | Kuondolewa darasani au eneo la mafunzo na karipio kali mbele ya kamati ya nidhamu | Onyo kwa maandishi kupitia kamati ya nidhamu | Kusimamishwa masomo kupitia kamati ya nidhamu |
| 3 | Kusuka nywele bandia, kupaka kucha rangi, kupaka wanja na kupaka rangi za mdomo | Kuondolewa darasani au eneo la mafunzo na karipio kali mbele ya kamati ya nidhamu | Onyo kwa maandishi kupitia kamati ya nidhamu | Kusimamishwa masomo kupitia kamati ya nidhamu |
| 4 | Nguo zinazoacha sehemu ya mwili wazi kama kitovu na kifua na kuonesha maungo | Kuondolewa darasani au eneo la mafunzo na karipio kali mbele ya kamati ya nidhamu | Onyo kwa maandishi kupitia kamati ya nidhamu | Kusimamishwa masomo kupitia kamati ya nidhamu |
| 5 | Kuvaa suruali mlegezo au imechanwa magotini | Kuondolewa darasani au eneo la mafunzo na karipio kali mbele ya kamati ya nidhamu | Onyo kwa maandishi kupitia kamati ya nidhamu | Kusimamishwa masomo kupitia kamati ya nidhamu |
| 6 | Makosa mengine yote ya mavazi yasiyo ruhusiwa | Kuondolewa darasani au eneo la mafunzo na karipio kali mbele ya kamati ya nidhamu | Onyo kwa maandishi kupitia kamati ya nidhamu | Kusimamishwa masomo kupitia kamati ya nidhamu |

# Sare za wauguzi na ukunga







# Sare za kada shirikishi za afya








## Nywele zinazoruhusiwa kwa wasichana/wanawake





## Nywele zinazoruhusiwa kwa wavulana/wanaume





Urefu wa suruali na viatu vinavyoruhusiwa kwa wavulana/wanaume





Viatu na socks vinavyoruhusiwa kwa wasichana/wanawake





# Masweta yanayoruhusiwa kwa kada zote





# Hijabu



